Wizara yakanusha kuingizwa mayai toka nje

Na Elizabeth Zaya

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi, imesema hakuna mayai kutoka nje ya nchi ambayo yameingizwa nchini kama ambavyo imedaiwa na kusambazwa kwenye mitandao ya kijamii.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, hakuna uingizaji wa mayai kutoka nje ya nchi uliosababisha kushuka kwa bei ya bidhaa hiyo katika ngazi ya mfugaji na sokoni.

"Juni 14, mwaka huu, Wizara iliona ujumbe ukizunguka kwenye mitandao ya kijamii kuhusu kuingia kwa mayai mengi nchini kutoka nje kiasi cha kusababisha kushuka kwa bei ya mayai mpaka kufikia Sh.4,000 kwa trei. Ujumbe huu ulikuwa ukisomeka 'soko la mayai DSM kitendawili.

"Baada ya kuona ujumbe huo, Juni 16, mwaka huu, wizara ilifanya uchunguzi kwenye maeneo makuu ya mikoa 26 nchini na baadhi ya wilaya ili kujiridhisha juu ya upatikanaji wa mayai.

Baada ya uchunguzi huo, ilibainika kwamba kinachoonekana ni upungufu wa mayai nchini ambao umesababisha bei ya bidhaa hiyo kupanda hadi kufikia Sh.12,000 kwa trei na si Sh. 4,000 kama ilivyoakuwa ikisambazwa kwenye mitandao.

"Taarifa zilizosambazwa ni uzushi na hazina ukweli wowote kwa sababu serikali ilishazuia uingizwaji wa kuku na mazao yake kutokana na tishio la uwapo wa ugonjwa wa mafua na ndege duniani. Wizara imekuwa ikitoa vibali maalum vya kuingiza vifaranga na mayai ya kutotolesha ya kuku wazazi. Kwa hiyo taarifa hizo za uzushi zipuuzwe," ilisema taarifa hiyo.

Ndaki alisema suala la uhaba wa vifaranga nchini linafanyiwa kazi na kwamba kufikia Septemba mwaka huu litakuwa limetatuliwa na kurudi katika hali ya kawaida.

Kuhusu ugonjwa wa homa ya nguruwe nchini, Ndaki alisema wizara imekuwa ikifanya juhudi kubwa kuudhibiti na kwamba mpaka kufikia mwishoni mwa Aprili, mwaka huu, katika mikoa mingi nchini hakukuwa na matukio ya ugonjwa huo.

"Januari 23, mwaka huu, nilitoa taarifa kwa umma juu ya uwapo wa mlipuko wa ugonjwa wa homa ya Nguruwe katika maeneo ya mikoa ya Mwanza, Kagera, Shinyanga na Dodoma na niliwaagiza wakuu wa mikoa, wilaya na wakurugenzi wa halmashauri, kusimamia utekelezaji wa masharti ya karantini zilizokuwa zimewekwa na wataalamu wa mifugo, nawashukuru sana kwa jinsi walivyosimamia kazi hiyo," alisema Ndaki.

"Juni Mosi, mwaka huu, katika Manispaa ya Morogoro kulijitokeza matukio ya nguruwe 14 kufa na uchunguzi wa kimaabara ulionyesha ni ugonjwa wa homa ya nguruwe.

"Tayari juhudi kubwa za kudhibiti zinaendelea ambazo ni pamoja na kuweka karatini ya kuingiza na kutoa nguruwe na mazao yake katika Manispaa hiyo na elimu inatolewa kwa wafugaji na wadau wengine kuhusu njia za kukinga ugonjwa usiingie kwenye mabanda ya mifugo hiyo. Mpaka kufikia juzi hali ya ugonjwa katika Manispaa ya Morogoro imedhibitiwa na hakuna kifo tena kilichotokea kwa Nguruwe," alibainisha Ndaki.

Nipashe uk. 8, Juni 20,2021

Scanned with CamScanner

Dawati la Jinsia kubadili mtazamo wa wanawake sekta ya uvuvi

Na Mwandishi Wetu

SERIKALI imesema uwepo wa Dawati la Jinsia katika Sekta ya Uvuvi kutasaidia kuimarisha usawa wa kijinsia pamoja na kuboresha uratibu wa serikali hususani uboreshwaji wa Sera ya Taifa ya Uvuvi juu ya mtazamo wa wanawake katika Sekta ya Uvuvi nchini.

Akimwakilisha Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Uvuvi Dk Rashid Tamatamah, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa wizara hiyo katika Sekta ya Uvuvi, Amos Machilika, wakati wa uzinduzi wa dawati hilo jijini Dodoma, alisema wanawake katika sekta ya uvuvi wanachukua nafasi kubwa na muhimu katika mnyororo wa thamani wa mazao ya uvuvi.

Machilika aliongeza kuwa mwezi Novemba mwaka 2019, serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi Sekta ya Uvuvi ilisaini makubaliano na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), kutekeleza mradi wa uwezeshaji wa utekelezaji wa mwongozo wa hiari wa kuhakikisha uvuvi mdogo unakuwa endelevu (SSF) katika muktadha wa uhakika wa chakula na kuondoa umasikini.

Aidha alifafanua kuwa ili kuwaunganisha na kuwatengenezea mazingira mazuri wanawake wote wanaojishughulisha na uvuvi katika sekta ya uvuvi nchini, Wizara hiyo kwa kushirikiana na FAO imeamua kuanzisha dawati la jinsia katika sekta ya uvuvi kwa ajili ya kutatua kero zinazowahusu wanawake na makundi yaliyo katika mazingira magumu katika sekta hiyo na kuzipatia utatuzi.

Alitaja baadhi ya kero hizo kuwa ni [illegible] kazi nzito na kulipwa [illegible] mdogo au kutolipwa kabisa, unyanyasaji wa kingono, ukosefu wa taarifa juu ya masoko ya bidhaa zao, ukosefu wa elimu juu ya ujasiriamali na usimamizi wa rasilimali fedha.

Kwa upande wa Ofisa Uvuvi wa Wizara hiyo, Abdi Hussein, kazi ya utambuzi wa idadi ya vikundi vya wanawake wanaojihusisha na uvuvi wapatao takriban 6,000 wizara iliunda Jukwaa la Wanawake wanaojihusisha na shughuli za uvuvi nchini (TAWFA) aidha wizara iliona ni vyema kuunda Dawati la Jinsia ili kuwafikia wanawake wote nchini na makundi maalum.

Katibu Msaidizi wa Jukwaa la Wanawake wanaojihusisha na shughuli za Uvuvi nchini (TAWFA) Fatuma Katula, alibainisha kuwa baadhi ya sheria zimekuwa zikimbana mwanamke, hivyo kupitia dawati la jinsia changamoto nyingi z tatatuliwa na lengo ni kufi mbali na kuongeza uchum wa nchi pamoja na nchi kuona kwamba kinapatik chakula sahihi na bora.

Scanned with CamScanner

UHARIBIFU

Ekari 200 zaliwa na mifugo Mkuranga

Elias Msuya, Mwananchi
emsuya@mwananchi.co.tz

Baadhi ya wakulima wa kijiji cha Kisegese wilayani Mkuranga, Mkoa wa Pwani wakiangalia ng'ombe wanaodaiwa kuwa wa Wamang'ati wakila mazao katika mashamba yao hivi karibuni. **Picha na Elias Msuya.**

Mkuranga. Zaidi ya ekari 200 za mashamba ya mpunga katika kijiji cha Kisegese wilayani Mkuranga Mkoa wa Pwani zimeliwa na mifugo inayomilikiwa na wafugaji wa kabila la Wamang'ati.

Mbali na uharibifu huo, wafugaji hao wanadaiwa kujeruhi watu wanne ndani ya mwezi mmoja.

Miongoni mwa wakulima waliopoteza mazao ni aliyekuwa Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), Jaji mstaafu Amir Manento ambaye pamoja na ndugu zake wamepoteza ekari 76 za mpunga.

"Tumewekeza fedha, mashine na nguvu nyingi kwenye kilimo cha mpunga, lakini wote umeliwa na ng'ombe," alisema Jaji Maneno kwa simu.

Mwananchi limefika katika kijiji hicho na kushuhudia makundi ya ng'ombe na punda wakiendelea kula mpunga ulio tayari kuvunwa, huku baadhi ya wakulima wakidai kutishwa na wafugaji hao kwa mikuki.

Wachungaji wa mifugo hiyo walikimbia na kuacha baada ya kuona wanakijiji wakifika shambani.

Hata hivyo, Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Filberto Sanga alipoulizwa kwa simu alisema wameshawaondoa wafugaji.

"Ni kweli kuna hilo tatizo, lakini tumeshachukua hatua ikiwa pamoja na kuwatoa wale wafugaji. Pili, tumeshawasiliana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, wameshatuma timu ya wataalamu wako huko sasa hivi," alisema DC Sanga.

Mwananchi linatambua kuwa aliyekuwa Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Rufiji, ambaye sasa ni Mkuu wa Polisi Mkoa (RPC) wa Dodoma, Onesmo Lyanga alifika kijijini hapo Juni 4, mwaka huu akiwa na Sanga baada ya kuzuka mapigano ya wakulima na wafugaji.

Hata hivyo, baada ya ujio huo, wakulima wanalalamika kuwa hakuna juhudi zilizofanywa, kwa kuwa wafugaji hao wameendelea kuwatisha na hatimaye kuharibu mazao yote yaliyokuwa shambani.

"Wakati RPC anakuja mashamba yaliliwa yameliwa kidogo, lakini walipoondoka, wafugaji wameendelea kuingiza ng'ombe mashambani, hata sasa ukienda shambani wapo wanaendelea kulisha bila wasiwasi," alisema Elisa Mnguruta, mmoja wakulima hao.

Mnguruta, anayeishi kitongoji cha Mindevu alimwambia mwandishi wa habari hizi kuwa alifika kijiji hicho miaka minne iliyopita kwa lengo la kuwekeza kwenye kilimo.

"Tulipohamia kijiji hiki miaka minne iliyopita tulilambiwa hakutakuwa na mifugo na tulitoa hela za kupimiwa mipaka, sasa inashangaa ieo mifugo imeruhusiwa," alisema.

Mbali na kuliwa mazao yake, Mnguruta amesimulia tukio la kuporwa Sh35 milioni na wafugaji hao walivamia nyumbani kwake [illegible] alipita" alisema.

tokea mgogoro baada ya mifugo kuvamia mashamba yetu. Tulikamata ng'ombe waliokula mazao, tukawaleta kijijini. Wafugaji walipokuja tulichukua ng'ombe sita kama fidia.

"Ila usiku wake walikuja wafugaji wakiwa na mikuki na mishale wakawachukua ng'ombe kwa nguvu na kupora begi langu lililokuwa na fedha," anasimulia.

Mnguruta anasema licha ya kuwa na bunduki hakuweza kuwakabili wafugaji hao, kwa sababu usiku huo alipata taarifa kuwa shamba lake limevamiwa, hivyo alikimbilia shambani.

Katika mgogoro huo, wakulima wanne walijeruhiwa, akiwemo Rashidi Kashindi aliyechomwa mkuki mgongoni.

Akisimulia tukio hilo, Salima ambaye ni mtoto wa Kashindi anasema baba yake alitoka kuwakabili Wamang'ati saa 5 usiku akiwa na panga.

"Nilisikia kelele watu wakiomba msaada, nikamwamsha baba, alipoamka akatoka nje huku ameshika panga, akakuta Wamang'ati wanafungua wale ng'ombe. Wakati huo wengine walivamia nyumbani kwa Mzee Mnguruta na kuanza kumpiga mkewe.

"Walipomwona baba wakaanza kumkimbiza, alipokaribia nyumbani akajikwaa akaanguka, ndipo walipomchoma mkuki wa mgongoni. Mdogo wangu naye alitoka kuwakabili Wamang'ati, lakini walimjeruhi mkononi na alikimbia mbali hakurudi siku hiyo,"

Sh35 mil

Fedha anazodaiwa kuporwa mkulima Elisa Mnguruta na wafugaji waliovamia nyumbani kwake.

200

Ekari za mazao zilizoliwa na mifugo katika kijiji cha Kisegese.

alisema.

Naye Neema Ndiu ambaye ni mke wa Mnguruta alisema wafugaji walivamia nyumbani kwao na kumkuta peke yake na kuanza kumpiga na kuondoka na begi lililokuwa la Sh35 milioni.

"Zilikuwa ni pesa tulizotumiwa na wateja wetu wa mpunga, zote zimekwenda. Mimi nimepigwa mpaka sasa siwezi kufanya kazi mwili wote unauma.

"Lakini cha ajabu, watuhumiwa tuko nao humu kijijini hawakamatwi. Wanajitapa kuwa wameshatoa donge nono kwa wakubwa.

"Tunahofia kwenda kuvuna kwa sababu tunatishiwa maisha," alisema Ndiu.

Mnguruta anasema walitoa taarifa kwa Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga na Kamanda wa Polisi wa Rufiji.

"Mkuu wa Wilaya alikuja na Polisi na wakaangalia hali ilivyotokea na kuahidi kuleta askari awasake wafugaji. Kweli kesho yake askari wa FFU wakaja, lakini hawakukamata mtu," alisema.

Aliendelea; "Mpaka sasa tumeshapoteza ekari 76 za mpunga na wakulima wengine wenye mashamba madogo pia wamepoteza mazao katika mashamba yao ambayo ukijumlisha tumepoteza zaidi ya ekari 200.

"Pia, tumeshambuliwa, mwingine kapigwa mkuki, mwingine kavunjwa mkono, wengine wamejeruhiwa sehemu mbalimbali. Tumemwambia DC na Polisi, lakini hatujapata msaada wowote," alisema Mnguruta.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rufiji, John Malulu alisema ili kuepusha migogoro kuna hatua za mchanganyiko za kiutawala hasa Kamati ya Ulinzi na Usalama. Vijiji, kata wameelekezwa kutenganisha wakulima na wafugaji, kwamba yawepo maeneo ya kulisha mifugo.

Kuhusu kukamata mifugo, alisema: "Kwenye mashauri ya kuharibu mali, mifugo siyo kielelezo. Kilichoharibiwa kinafanyiwa tathmini na wataalamu wa idara nyinginezo, ispokuwa ni muhimu kuainisha kuwa hiyo mifugo ni ya nani, kwa sababu mwenye mifugo ndiye mtuhumiwa.

Kwa upande wake, Yasin Manento alisema wafugaji walimvamia katika shamba lake wakati wakiwa kwenye harakati za kuvuna mpunga.

"Walikuja Wamang'ati wanne wakiwa na makundi ya ng'ombe wapatao 300 hivi, wakawaingiza kwenye shamba langu.

"Nilijaribu kuwafukuza, lakini mmoja wao alinitishia kwa mkuki na fimbo, akasema 'ninyi ndiyo tunaowatafuta'. Ikabidi niwaachie waendelee kulisha. Wavunaji waliokuwa shambani wamerudi tu na visu bila chochote," alisema Manento.

Wakulima wengine waliozungumzia sakata hilo walisema limesababishwa na kijiji cha jirani kinachoitwa Mgoi kuruhusu wafugaji ambao sasa wamehamia kijiji cha Kisegese.

Kondo Mkorongo aliyeishi kijijini hapo tangu mwaka 1979 alisema: "Baada ya kijiji cha Changoi kukaribisha wafugaji, tatizo ndipo lilipoanza, kwani tuliwekewa hadi mabango na wafugaji wakitutaka tuhame kwenye mashamba yetu.

Naye Mohamed Mngosongo alisema amepoteza ekari 10 za mpunga kutokana na mifugo hiyo.

Kauli hiyo inaungwa mkono na Omari Rashid Makubi, aliyeanza kilimo kijijini hapo mwaka 2001 akisema mifugo kijijini hapo imesababisha umaskini mkubwa.

Kwa upande wake, Kasiga Shakamshiri alisema wanakatishwa tamaa na Serikali kwa kushindwa kutatua mgogoro huo, akisema wamewekeza fedha na nguvu zao ili kujiajiri.

"Tumeamua kuja kijijini kujiajiri, lakini tunachoambulia ndiyo hiki, hivi Serikali inataka sisi twende wapi?" alihoji.

Mwenyekiti wa kijiji cha Kisegese, Daudi Tumbo alikiri kuwepo kwa kadhia hiyo, akisema jukumu lake ni kuripoti matukio kwa viongozi husika.

"Hata hapa unaponiona nimetoka kwenye mkutano wa halmashauri na nimewaeleza kuhusu uvamizi wa wafugaji.

"Kimsingi hawa wafugaji ni wavamizi kwa sababu kijiji chetu hakina wafugaji katika mpango wa matumizi ya ardhi," alisema.

KAULI YA POLISI

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rufiji, John Malulu amekiri kuwepo kwa migogoro ya wakulima na wafugaji katika eneo lake, lakini akasema Polisi ni taasisi ya mwisho kushughulikia suala hilo.

Alisema hana takwimu za watu waliokamatwa kwa kuwa yuko safarini, lakini kila mgogoro ukitokea kuna watu wanakamatwa.

Ulinzi na Usalama. Vijiji, kata wameelekezwa kutenganisha wakulima na wafugaji, kwamba yawepo maeneo ya kulisha mifugo.

Scanned with CamScanner

Waziri ataka kuwapo bima na mikopo wavuvi, wafugaji

Na Augusta Njoji, DODOMA

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amezitaka taasisi za bima na za kifedha kuwakomboa wafugaji na wavuvi kwa kuwawezesha kuwa na bima ya kulinda vitega uchumi vyao ili wakopesheke.

Alisema hayo juzi akifungua kikao cha wadau wa dawati la sekta binafsi ambalo lipo chini ya wizara hiyo.

Alisema wafugaji na wavuvi wamekuwa wakikabiliwa na kero ya kutokukopesheka kirahisi na taasisi za kifedha na hivyo kuwafanya washindwe kuitumia fursa ya mikopo kukuza mitaji yao.

Naibu Waziri huyo alisema kutokana na hali hiyo Wizara imeona ni vema kuwakutanisha wadau kujadili na kupata suluhisho kwa wakulima na wafugaji kuwa na bima.

"Mifugo na samaki ni uwekezaji na ni biashara kubwa hivyo taasisi hizi za bima na fedha lazima ziwe na mtazamo huo na kwamba kufanya kazi na wafugaji na wavuvi kutawaletea tija pia,"alisema.

Alifafanua kuwa lengo ni kuhakikisha uwekezaji na biashara kwenye sekta za mifugo na uvuvi zinakua na mchango wake katika kipato cha mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Alishauri taasisi za fedha kuangalia uwezekano wa kupunguza riba kwenye mikopo ili wafugaji na wavuvi wakopesheke kirahisi.

Kaimu Katibu Mkuu anayeshughulikia sekta ya Mifugo, Dk. Bedan Masuruli, alisema sekta za mifugo na uvuvi zinahitaji kuendelezwa na moja kitu kinachotakiwa ni mitaji.

Kwa upande wake, Mratibu wa Dawati la Sekta Binafsi kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Stephen Michael, alisema dawati lilifuatilia upatikanaji wa bima kwa wafugaji ili kuwasaidia wafugaji na wavuvi kupata mikopo.

"Shirika la Bima la Taifa (NIC), limetoa bima kwa vyama vya ushirika vya wafugaji vitatu na vyama vya ushirika vya wavuvi vitatu,"alisema.

Kaimu Mkurugenzi wa Mipango, Utafiti, na Maendeleo ya Masoko ya Bima Tanzania, Muyengi Zakaria, alisema wameshazielekeza kampuni zote za bima nchini waandae bidhaa ambazo zinakidhi mahitaji ya wafugaji na wavuvi.

Nipashe uk.9, Juni 20,2021

Scanned with CamScanner

No swine fever, govt assures public

By HILDA MHAGAMA

THE government has assured the public that there is no spread of African swine fever in Dar es Salaam, as it has been reported recently.

Livestock and Fisheries Minister, Mashimba Ndaki (pictured) said yesterday in Dodoma that the deaths of 298 pigs reported are not related to the viral disease.

"It is true that on June 9, 2021 the ministry received information on the presence of Swine Flu in Dar es Salaam, however after investigating two farms in the city we found the death of 298 pigs was not caused by the said disease," he said.

He further said the ministry dispatched a team of experts and after a thorough examination of the remaining pigs in the fields, including taking samples and testing them in the laboratory, the results didn't not show any signs of Swine Flu.

Mr Ndaki warned rumour mongers who scare swine-breeds and the general public that there is Swine Flu in Dar es Salaam.

"We continue to monitor all pig farms in Dar es Salaam to see if symptoms of the disease appear but so far there is no single sign of the disease," he said.

According to the minister, on June 1, 2021, in Mwanyamala Municipality, 14 pigs died with the study showing that they died of swine flu.

"We made various efforts to prevent the problem from spreading, including imposing restrictions on the relevant areas for the import and export of pigs and their products in Mwanyamala municipality from June 3, this year. We also provided education to breeders and other stakeholders on the best ways to prevent the disease from spreading," he explained.

African swine fever is a highly contagious and deadly viral disease affecting both domestic and feral swine of all ages, it is not a threat to human health and cannot be transmitted from pigs to humans.

The disease is found in countries around the world, particularly in sub-Saharan Africa. More recently, it has spread through China, Mongolia and Vietnam, as well as within parts of the European Union.

Daily News uk.4
Juni 20,2021

Scanned with CamScanner